# ZABURI
## Zb117
### Siku ya Mungu ya nne ya Paska

**Musique: GRACE MUSHAGALUSA Fabrice**




1. Mshukuruni Bwana kwani ndiye mwema,
   kwani wema wake ndio wa milele;
   wenye kumwabudu Bwana waseme;
   kweli wema wake ndio wa milele.

2. Bora kumkimbilia Bwana,
   kuliko kumwamini mwanadamu;
   bora kumkimbilia Bwana,
   kuliko kuwaamini wakuu.

3. Jiwe walilokataa wajengaji
   limekuwa jiwe la pembe.
   Ndio jambo alilofanya Bwana
   nasi twaliona ni ajabu.

4. Wewe ndiye Mungu, ninakushukuru;
   wewe Mungu wangu, ninakutukuza,
   Msukuruni Bwana kwani mwema,
   kwani wema wake ndio wa milele.